

Kuweka Pesa Akiba

Karatasi la uhakika wa muongozo wa pesa zako

Bona ni wazo mzuri kuweka akiba pesa?

Watu huweka pesa akiba kwa sababu wanataka kununua kitu wakati ujao (lengo la kuweka akiba) au kuwa na pesa kama kitu kikienda vibaya. (pesa za dharura)

Ninawezaje kuanza kuweka pesa akiba? Jiulize maswali haya:

- ▶ Nini ninachotaka kuweka akiba?
- ▶ Ni Pesa ngapi nahitaji kuweka akiba?
- ▶ Ni Pesa ngapi naweza kuweka akiba kila wakati ninapolipwa?
- ▶ Itachukua muda gani kufikia lengo langu?

Kuwa na mpango ili uweze kufikia lengo lako la kuweka akiba.

Mara tu unapoanza kuweka akiba, weka pesa zako kwenye benki, umoja wa kusadiki au ujenzi wa jamii (ili usitumie pesa zako ulizoweka akiba kwa ajili ya mambo mengine).

Kumbuka

- ▶ Kuweka akiba pesa zako ni kuweka pesa zingine kado ili kuzitumia wakati ujao.
- ▶ Kuweka akiba pesa hukusaidia wewe kuvilipia vitu vinavyogharimu pesa nyingi.
- ▶ Kuwa na pesa akiba hukusaidia wewe wakati unapokuwa na matumizi ya kighafla au yasiyotarajiwa.

Wapi kupata usaidizi na maelezo zaidi

Kwa maelezo zaidi kuhusu kuweka akiba pesa, tembelea tuvuti ya MoneySmart, www.moneysmart.gov.au, au pigia Afisa wa Huduma ya Maelezo ya Kifedha kutoka Centrelink kwenye simu 13 23 00 ili ufanye mpango wa taarifa ya gharama.



Fran anaanza kuweka pesa akiba kwa zharura

Fran ni mama anyeishi peke yake na watoto wawili wachanga. Yeye hufanya kazi ya muda kama mpokeaji kwenye afisi. Yeye anazo pesa za kutosha kwenye pochilake kwa ajili ya chakula na bili lakini mara nyingi anapata wasiwasi kama kitu kinahitajika kutengenezwa ambacho yeye labda hawezi kutosheleza kulipia.

Fran huamua kutayarisha taarifa ya gharama. Yeye huketi chini usiku moja na kuandika mapato yake na matumizi.

Ingawa Fran anabaki sha pesa kidogo tu baada ya kutimiza mahitaji yake ameamua kuwa yeye anaweza kuanza kuweka pesa kidogo kwenye akiba. Ameonelea njia moja ya kupunguza matumizi yake ni kupunguza vikombe vya kahawa anavyokunywa akiwa kazini. Kama akinunua kahawa 1 pekee badala ya 3 kwenye juma anaweza kuokoa \$10 kwenye juma. Fran anafikiria kuwa hii itakuwa ngumu lakini yeye atajaribu.

Juma la kwanza Fran alitumia kahawa 2, na kwenye juma zilizofuatia yeye aliweza kuzoea kununua kahawa 1 pekee. Kila juma Fran aliweza kuona akaunti ya akiba ikikua. Hii ilimfanya afurahie.

Fran aliamua kuweka \$10 kil juma kwenye akaunti ya akiba kwa ajili ya mambo ya dharura. Jinsi hii yeye atakuwa na pesa za kutosha kulipia matumizi yasiotarajiwa, vitu yeye anafaa kulipia kwa ghafla.

Miezi miatatu baada ya kuanza akaunti ya akiba kwa ajili ya dharura, Betri la gari la Fran liliwacha kufanya kazi na yeye alihitaji ingine mpya. Hapo mbeleni, yeye hangukuwa na pesa za kutosha ili kununua betri mpya. Sasa, Fran ana \$120 kwenye akaunti ya akiba kwa ajili ya dharura na aliweza kununua betri mpya, amabayo ilimgharimu \$90, mara moja. Hii iliwezekana tu kwa sababu alikuwa na pesa za kutosha kwenye akaunti yake ya akiba ya kutumia wakati wa mambo ya dharura.

This page has been intentionally left blank.